



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA (TanTrade)



MAFANIKIO YA (TanTrade) KATIKA KUKUZA BIASHARA NDANI NA NJE YA NCHI

IDADI YA WAFANYABIASHARA

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade anasema mamlaka hiyo imefanikiwa kuratibu programu tisa za mafunzo kwa wafanyabiashara ili kuimarisha uwezo wa kujiendesha kiushindani na kutumia ipasavyo fursa za masoko zinazopatikana.

MASOKO YALIYOTAFUTWA

Mkurugenzi huyo anasema katika kipindi cha miaka miaka miwili (2021-2023), TanTrade imeratibu matukio mbalimbali ikiwemo programu za utafiti, kongamano, misafara ya kibiashara, maonesho na mikutano.

BIDHAA ZILIZOTAFUTIWA MASOKO



IDADI YA WAFANYABIASHARA



Tan Trade YAJIVUNIA



facebook.com/TanTradetz



youtube.com



instagram.com/tantradetz

TanTrade katika kukuza biashara ndani na nje ya nchi

NA MWANDISHI WETU

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ilianzishwa kwa Sheria Namba 4 ya Mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho na The Business Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 3 of 2012.

Sheria hiyo ilifuta Sheria Namba 5 ya mwaka 1978 iliyoanzisha Bodi ya Biashara ya Nje (Board of External Trade - BET) na Sheria Namba 15 ya mwaka 1973 iliyoanzisha Bodi ya Biashara ya Ndani (Board of Internal Trade - BIT).

Hivyo, majukumu ya iliyokuwa Bodi ya Biashara ya Ndani na Bodi ya Biashara ya Nje sasa yako chini ya TanTrade. TanTrade ina jukumu la kukuza na kuendeleza biashara ya ndani na nje ya nchi ili kuimarisha biashara yenye tija katika maendeleo ya kiuchumi, biashara yenye tija katika maendeleo ya kiuchumi.

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Khamis anaeleza kuwa dira ya mamlaka hiyo ni kuwa kitovu cha ufanisi wa hadhi ya kimataifa (world class focal point) katika kuendeleza na kukuza uchumi wa Tanzania kupitia Biashara.

Pia, anabainisha kwamba dhamira ya TanTrade ni kutafuta fursa za kibiashara kwa kampuni za Kitanzania na kuziunganisha na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Latifa anabainisha kuwa kauli mbiu ya TanTrade ni "TanTrade Fostering Business" (TanTrade kwa Uimarishaji Biashara).

MAJUKUMU YAKE KISHERIA

Katika kutimiza azma ya kuendeleza na kukuza biashara nchini, Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade anasema mamlaka hiyo inatekeleza majukumu yafuatayo kwa mujibu wa Sheria: -

“

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Khamis anaeleza kuwa dira ya mamlaka hiyo ni kuwa kitovu cha ufanisi wa hadhi ya kimataifa (world class focal point) katika kuendeleza na kukuza uchumi wa Tanzania kupitia Biashara.

Kuisha Serikali kwenye masuala ya kuunda, kuendeleza, kusimamia na kutekeleza Sera na Mikakati ya biashara;

ii. Kutangamanisha na Kudhibiti maendeleo ya Soko la Ndani (Integrate and Regulate the Domestic Market Development);

iii. Kushirikiana na Taasisi wezeshi katika uwekezaji ili kuhakikisha uwekezaji unalenga katika uongezaji thamani;

iv. Kusaidia uwekaji wa mazingira rafiki kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini ili kuyafikia masoko ya ndani, kikanda na kimataifa;

v. Kutambua na kushauri mbinu bora za kutatua changamoto zinazokwamisha maendeleo ya biashara katika mnyororo wa thamani;

vi. Kutoa ushauri na mafunzo kwa Jumuiya ya Wafanyabiashara juu ya namna bora ya kusimamia shughuli za biashara ya ndani na ya nje;

vii. Kujenga na kukuza utamaduni wa kuuza bidhaa nje (export culture) kwa wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa kwa njia mbalimbali;

viii. Kuanzisha, kutunza na kuendeleza kanzidata (database) ya taarifa za biashara nchini;

ix. Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza; na kushauri kuhusu utaalamu wa uendelezaji na usimamizi wa miundombinu ya uhifadhi wa bidhaa (warehousing facilities);

x. Kukuza na kuwezesha uanzishwaji wa miundombinu ya Maonesho nchini;

xi. Kuanzisha na kuendeleza vituo vya biashara ndani na nje ya nchi;

xii. Kuratibu Maonesho ya Biashara, Misafara na Mikutano ya wafanyabiashara; mawasiliano miongoni mwa wafanyabiashara, kufanya tafiti za Masoko, Uhakiki wa mahitaji na kuendeleza bidhaa nchini;

xiii. Kuandaa na kusambaza taarifa na masuala mbalimbali yahasuyo biashara yanayofanywa na Mamlaka, mtu au Taasisi kwenye machapisho na vyombo vya habari kwa lengo la kukuza biashara kwa ufanisi na utekelezaji wa Sera na mikakati mbalimbali inayohusiana na biashara;

xiv. Kutoa ushauri na kuisaidia Serikali na Taasisi mbalimbali kuhusu kuchagua na kuajiri Mshauri Mwelekezi



Mkurugenzi Mkuu TanTrade, Latifa Khamis

wa biashara wa ndani na nje ya nchi kwenye masuala ya uendelezaji biashara;

xv. Kumruhusu mtu yoyote, Taasisi au Shirika linalotaka kuandaa Maonesho ya kimataifa ndani na nje ya Tanzania na kuwezesha, kusaidia, na pale inapobidi kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu kwa wahusika;

xvi. Kutathmini na kusimamia mifumo ya biashara na utendaji wake; na

xvii. Kufanya tafiti za kimasoko.

Anaeleza kwa mujibu wa sheria hiyo, TanTrade ilipewa mamlaka ya udhibiti, utendaji na kutoa ushauri wa kukuza na kuendeleza biashara ya Tanzania ndani na nje ya nchi ili kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Hivyo, lengo la kuanzishwa kwa Taasisi bado ni muhimu na linaendelea kutekelezwa.

MASOKO YALIYOTAFUTWA

Mkurugenzi huyo anasema katika kipindi cha miaka miaka miwili (2021-2023), TanTrade imeratibu matukio mbalimbali ikiwemo programu za utafiti, kongamano, misafara ya kibiashara, maonesho na mikutano ya kuunganisha wazalishaji na wanunuzi kwa lengo la kupata masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini. Kufuatia uratibu huo, masoko yafuatayo yalipatikana:

Jedwali Na 1: Orodha ya masoko yaliyoratibiwa katika kipindi cha 2021-2023

Na	Soko / Nchi	Kampuni zilizoshiriki	Mazao ya kipaumbele katika soko husika
	Kenya	54	Bidhaa vyakula, nafaka, mbao na mashudu
	Uturuki	50	Pamba, ngozi, viungo na mbogamboga
	Comoro	15	Nafaka, mifugo, mbogamboga, vifaa vya ujenzi, vyomba vya majumbani na matunda
	Saudi Arabia	9	Kokoa, Kahawa, chai, Korosho, nyama na asali
	Oman	300	Nyama, nafaka, mbegu za mafuta, mbogamboga na matunda,

Yajivunia mafanikio

DRC	271	Mahindi, maharage, mtama, mchele, unga wa mahindi, bidhaa za viwandani na huduma ya teknolojia
Sudani Kusini	55	Mahindi, maharage, mtama, mchele, unga wa mahindi, bidhaa za viwandani, elimu, teknolojia, afya, viwango vya ubora
Afrika Kusini	16	Kahawa, korosho, asali, utalii, bidhaa za chuma na vifaa vya umeme
Malawi	150	Kilimo, uvuvi, uchumi wa bluu, uzalishaji utalii, huduma za fedha, uchukuzi, miundombinu, mawasiliano, madini, elimu na afya.

Makubaliano ya kibiashara katika nchi ya Sudani ya Kusini yaliyopatikana ni pamoja na Kampuni ya L&K International ya nchini Sudani Kusini imeonesha nia ya kununua mayai trei 350 kwa wiki kutoka Tume ya Ushirika ya Tanzania; SUMA JKT imepata kampuni mbili za Sudani Kusini zilizooneshwa nia ya kununua mahindi...

Tan Trade YAJIVUNIA MAFANIKIO

Kupitia matukio hayo, Latifa anasema baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa na mamlaka hiyo ni pamoja na:

Kusaini mkataba wa Makubaliano (MoU) kati ya Tanzania na Afrika Kusini ili kuimarisha ushirikiano katika sekta za viwanda, biashara, mafunzo ya kitaalamu kati ya nchi hizi;

Makubaliano ya kibiashara kati ya kampuni za Tanzania na Afrika kusini ikiwemo teknolojia ya ujenzi wa barabara kati ya Kampuni ya Ibra Contractors ya Tanzania na Pioneer group LLC ya Afrika Kusini, kununua karafuu na mafuta ya manukato kati ya Shirika la Biashara la Zanzibar na Kampuni ya Ndazalama Bonding ya Afrika Kusini; Oda ya ununuzi wa Korosho tani 150 kwa Kampuni ya Akros Cashew Factory Limited ya Tanzania kwenda Kampuni tano (5) za Afrika Kusini (Pretoria Cashew, We Nuts, Miente Manufacturing, Real Food na Soul & Earth Pty Ltd) na kampuni 8 za Afrika Kusini zilioneshwa nia kushiriki maonesho ya DITF 2023;

Makubaliano ya kibiashara katika nchi ya Sudani ya Kusini yaliyopatikana ni pamoja na Kampuni ya L&K International ya nchini Sudani Kusini imeonesha nia ya kununua mayai trei 350 kwa wiki kutoka Tume ya Ushirika ya Tanzania; SUMA JKT imepata kampuni mbili za Sudani Kusini zilizooneshwa nia ya kununua mahindi, maharage na mtama zaidi ya tani 1,000; na Kampuni ya Asa Agribusiness kutoka Tanzania imepata oda ya kuuza tani 400 za maharage.

Sambamba na hiyo, anasema mamlaka inaratibu majukwaa yanayotoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kutangaza bidhaa na kukutana na wanunuzi.

Katika kipindi cha miaka miwili, anabainisha kuwa jumla ya washiriki 6,700 wa ndani na nje ya nchi na jumla ya watembeleaji wapatao 566,658 walitembelea Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam.

Anayataja mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kutambua fursa, kujifunza mbinu za kiushindani, kukutana na wanunuzi, kupokea ushauri na maoni kutoka kwa wateja wa bidhaa na huduma mbalimbali, kupata uzoefu kutoka kwa kampuni na Taasisi zenye uzoefu mkubwa Kibiashara kama inavyobainishwa kwenye jedwali namba 2 hapa chini.

Jedwali 2: Muhtasari wa Uratibu wa Maonesho ya DITF 2021-2023		
	2022 (46th DITF)	2023 (47th DITF)
Kampuni za Ndani	2,975	3,233
Kampuni za Nje	225	267
Jumla ya Washiriki	3,200	3,500
Idadi ya nchi	23	19

Watembeleaji	265,957	300,701
Ajira zilizozalishwa	11,650	11,869
Mauzo ya papo kwa papo (TZS)	3,592,500,000	3,949,50 0,000
Maulizo ya Kuagiza Bidhaa nje ya nchi (TZS) (Imports)	5,738,615,000	5,143,000,000
Maulizo ya Kuuza Bidhaa nje nchi (TZS) (Exports)	5,088,980,000	3,616,000,000
JUMLA YA MAULIZO (TZS)	10,827,595,000	8,759,000,000

Kadhalika, anaeleza kuwa mamlaka hiyo pia inashirikiana na ofisi za Mikoa kuratibu maonesho ya kisékta ambapo jumla Wafanyabiashara 1,776 walishiriki Zanzibar na katika Mikoa ya Geita, Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma, Pwani, Tanga, Manyara, Morogoro na Dar es Salaam.

Kadhalika, mkurugenzi mkuu huyo anabainisha kuwa wadau wa viwanda wapatao 731 (Taasisi wezeshi na viwanda vidogo, vya kati na vikubwa) walifanikiwa kushiriki maonesho ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania. Maonesho haya yoe yalitoea fursa kwa kampuni na Taasisi kujitangaza, kuuza bidhaa zinazozalishwa nchini, kuongeza uelewa kwa Watanzania juu ya bidhaa hizo na kutoa hamasa ya kuzitumia.

Aidha, ili kuhakikisha maonesho yanayoratibiwa nchini yanatoa fursa kwa wazalishaji kupata masoko, anasema TanTrade imetoa ushauri wa uratibu wa maonesho 15 yaliyoratibiwa na Kampuni za ndani na nje ya nchi.

BIDHAHA ZILIZOTAFUTIWA MASOKO NA MAPATO YALIYOPATIKANA

Kufuatia uratibu wa shughuli za ukuzaji biashara zinazoratibiwa na TanTrade zimewezesha bidhaa mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 1,455,649 kuuzwa kwenye masoko ya nje ya nchi. Baadhi ya bidhaa hizo zinaonyeshwa kwenye mchanganuo ufuatayo:

Jedwali 3: Mchanganuo wa baadhi ya bidhaa za mazao ya kilimo zilizouzwa

Thamani ya mauzo ya bidhaa za kilimo (US \$000)				Nchi zinazoongoza kwa kununua bidhaa		
Bidhaa	2021	2022	Jumla miaka 5	1	2	3
Nyama	29,228	55,673	84,901	Qatar	UAE	Oman
Mchele	301,987	183,525	485,512	Uganda	Rwanda	Kenya
Soya	75,474	32,740	108,214	Rwanda	India	China
Karanga	14,358	22,230	36,588	China	Netherlands	Indonesia
Parachichi	10,923	20,996	31,919	Netherlands	UAE	South Africa
Pilipili	734	2,218	2,952	India	Ujerumani	Iran
Muhogo	2,370	3,899	6,269	Uganda	Brundi	China
Mahindi	91,546	88,949	180,495	Kenya	Rwanda	Uganda
Karafuu	51,783	42,120	93,903	Singapore	Indonesia	India
Asali	1,283	1,401	2,684	Ujerumani	Marekani	Ireland
Mbegu za maboga	11,119	12,026	23,145	Uholanzi	Congo DRC	China
Korosho	163,945	234,790	398,735	India	Vietnam	China
Zabibu	245	87	332	Kenya	Ghana	Comoros
Jumla Kuu			1,455,649			

Mafanikio ya TanTrade

MIKATABA/MAKUBALIANO YA BIASHARA

Anaeleza kuwa mamlaka hiyo inafuatilia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kibiashara iliyosainiwa katika matukio mbalimbali yaliyoratibiwa na TanTrade.

Katika kipindi cha miaka miwili jumla ya mikataba 46 yenye thamani ya TZS. 17.53 Trillion kati ya hiyo jumla ya mikataba 11 yenye thamani ya TZS. 4,497,584,960 imetekelezwa ambayo ilihusisha:-

Mauzo ya mchele tani 60 zenye thamani ya TZS. 136,800,000 ziliuzwa na Kampuni ya Kibu Agri Business kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko;

Mauzo ya mchele tani 90 zenye thamani ya TZS. 219,750,000 ziliuzwa na Kampuni MT & David Company Limited kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko;

Mauzo ya mahindi tani 53 zenye thamani ya TZS. 47,476,000 ziliuzwa na Kampuni Izna Farm Tanzania Limited kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko;

Huduma ya mafunzo ya uendeshaji mitambo yenye thamani ya TZS. 41, 000,000 yaliyotolewa kwa Chama cha Waokaji Tanzania (TBA) yaliyotolewa na Chuo cha Biashara (CBE) kwa kushirikiana Shirika la Viwanda vidogo vidogo (SIDO) kuhusu usimamiaji wa biashara

(Business Management) kwa wajasiriamali 70 na mafunzo ya uendeshaji mitambo kwa wajasiriamali 140 wa tasnia ya Uokaji;

Makubaliano yenye thamani ya Dola za Kimarekani 515,700 ikiwa ni sawa na TZS. 1,204,159,500 kati ya Kampuni ya East Africa Commercial and Logistics Ltd ya Dar es Salaam kuizua kontena 20 za mbao kwa ajili ya urembo wa sakafu na kuta za nyumba kampuni ya EFL Company ya Dar es Salaam. Hadi sasa, 2022, kontena 7 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 195,966 ikiwa ni sawa na thamani ya TZS. 457,580,610 zimeuzwa.

Makubaliano yenye thamani ya Dola za Kimarekani 579,000 ikiwa ni sawa TZS. 1,351,965,000 kati ya Kampuni ya Shandong Sishui Haiyon Food Processing Machine Co. Ltd ya China kuuzia Seti 100 za machine ya kukoboa na kusaga kwa Kampuni ya Halce Group Ltd ya China. Jumla ya mashine 46 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 266,340 ikiwa ni sawa na thamani ya TZS. 621,903,900 zimekwishauzwa;

Makubaliano yenye thamani ya Dola za Kimarekani 364,500 ikiwa ni sawa na TZS. 851,107,500 kati ya Shandong Jin Hua Iron & Steel Co. Ltd ya China kuizua tani 27 za coil za mfumo wa vyombo vya ubaridi Kampuni ya GSB Mat Doors Ltd ya Tanzania. Mpaka sasa, mzigo wa tani 12 wenye thamani ya Dola za Kimarekani 167,670 ikiwa ni sawa na thamani ya TZS. 391,509,450 zimeuzwa;

Makubaliano yenye thamani ya Dola za Kimarekani 1,130,000 ikiwa ni sawa TZS. 2,638,550,000 kati ya Shandong Wuzhen Group Co.Ltd kuuzia maguta yenye injini Kampuni ya Chico Co.Ltd ya Tanzania. Hadi sasa maguta 200 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 339,000 ikiwa ni sawa na thamani ya TZS. 791,565,000 yameuzwa;

Makubaliano yenye thamani ya Dola za Kimarekani 5 Million ambayo ni sawa na TZS. 11.6 Billioni, kati ya STAMICO na Buhemba Gold Company Ltd wa uchorongaji wa mita 10,000 za Diamond Drilling (DD) na mita 30,000 za Reverse Circulation (RC) yalisainiwa. Hadi sasa awamu ya kwanza uchorongaji wa diamond drilling - DD (1450m) na reverse circulation RC (4000m) ukiwa na thamani ya Dola za Kimarekani 725,000 sawa na TZS. 1.69 bilioni umekamilika; na

Makubaliano yenye thamani ya Dola za Marekani 200 Million ambayo ni sawa na TZS. 4.6 Trillion kati ya STAMICO na ACME Consultants Engineers PTE Ltd ya kufanya Utafiti na Uchimbaji wa Madini ya metali nchini. Hadi sasa Kampuni ya ACME imeanza utekelezaji wake kwa kukusanya taarifa mbalimbali zinazohusu madini katika maeneo ya wachimbaji wadogo mikoa ya Shinyanga - Segese, Geita - Busolwa, na Ikuzi.

Kadhalika, anaeleza kuwa mamlaka iliunganisha wazalishaji 200 wa zabibu na viwanda 13 vya kusindika zabibu jijini Dodoma ambapo iliwezesha kupata soko la jumla ya tani 2,500 za zabibu zenye thamani ya Shilingi 3 bilioni zilizokuwa zimekosa soko kufuatia ongezeko la mavuno. Wakulima walionufaika ni wa Vijiji Mpunguzi, Mkulabi, Matumbulu, Hombolo, Chibelele, Makang'wa, Mvumi na Veyula;

THAMANI YA TZS. 791,565,000

Makubaliano yenye thamani ya Dola za Kimarekani 1,130,000 ikiwa ni sawa TZS. 2,638,550,000 kati ya Shandong Wuzhen Group Co.Ltd kuuzia maguta yenye injini Kampuni ya Chico Co.Ltd ya Tanzania. Hadi sasa maguta 200 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 339,000 ikiwa ni sawa na thamani ya TZS. 791,565,000 yameuzwa;

MASOKO TARAJIWA

Kwa mujibu wa uchambuzi wa takwimu katika tafiti za ndani za Tantrade na mfumo wa ITC, anasema bidhaa za Tanzania zinazohitajika kwa wingi nje nchi na hazijaweza kuuzwa kwa kiwango kinachohitajika ni pamoja na dhahabu, vito, korosho, mchele, ufuta, mbaazi, kahawa, denguu, matunda ikiwemo parachichi, asali, nyama ya ng'ombe, soya, muhogo, ndizi, nafaka na mbao.

Latifa anafafanua kuwa nchi ambazo zinahitaji bidhaa hizi ni pamoja na India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uswisi, Vietnam, Afrika Kusini, China, Kenya, Uganda, Rwanda DRC, Pakistani, Japani, Marekani, Oman, Qatar, Kuwait na Saudi Arabia

Jedwali Na.4: Bidhaa zenye Fursa kubwa kwenye Masoko ya Nje

Na	Bidhaa	Mauzo Halisi (milioni \$)	Uwezo wa Kuuza Nje milioni \$
	Dhahabu	2,100	3,400
	Korosho	306	819
	Mchele	151	317
	Sesame	152	207
	Mbaazi	95	201

	Kahawa	157	171
	Dengu	64	154
	Almasi	44	136
	Vifungashio vya mifuko	27	86
	Pamba	63	76

Chanzo: ITC 2023 - Export Potential Map

Ili kuweza kunufaika na fursa hizi za uhitaji wa bidhaa katika masoko ya nje, TanTrade inashirikiana na Ofisi za Ubalozi za Tanzania nje ya nchi ili kutafuta masoko na kufungua fursa za biashara.

UTOAJI WA TAARIFA ZA BIASHARA

Mamlaka inaendelea kuimarisha jitihada za ukusanyaji, uchambuzi, uhifadhi na usambazaji wa taarifa za biashara ili kuweza kuwafikia wadau wengi wa biashara kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mikutano, vyombo vya habari, tovuti, majarida, machapisho, mitandao ya kijamii na ujumbe wa simu za mkononi. Hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni pamoja na:-

Kuongeza wigo wa usambazaji wa taarifa za biashara kutoka wastani wa idadi ya watumiaji 20,000 mwaka 2021 na kufika 61,233 mwaka 2022. Taarifa zinazosambazwa ni pamoja na mwenendo wa bei za mazao na bidhaa za viwandani za kila wiki na mwezi, fursa za masoko, taratibu za kufanya biashara na kupata vibali vya kusafirisha bidhaa kupitia mfumo wa taratibu za ufanyaji biashara (Trade Portal <https://trade.tanzania.go.tz/>);

Kufanya uchambuzi wa mahitahi ya soko ikiwa ni pamoja na kufamu viwango vya ubora na taratibu za kuingiza bidhaa katika nchi husika hususani kwa bidhaa za parachichi, soya, viungo, asali, mbogamboga, nafaka, muhogo na nyama.

Kuhushia taarifa katika Mfumo wa Taarifa wa Taratibu za Ufanyaji Biashara nchini (Tanzania Trade Portal) wenye watumiaji 13,908 na watembeleaji 34,629 kwa lengo la kuongeza taarifa za usafirishaji wa mazao ya nyuki kwenda nje ya nchi (Export Procedures);

Kukamilisha mpango wa kurahisisha (simplify) taratibu za usajili, leseni na vibali kwa kuonisha mifumo ya ATMIS na BRELA ili kuruhusu kupata taarifa za makampuni/biashara (kama vile; wanahisa, wakurugenzi, mtaji wa hisa, shughuli zilizosajiliwa) kwa kutumia leseni ya biashara au nambari za utambulisho wa mlipa kodi (TIN) na Tax clearance;

Uchambuzi wa fursa za biashara kati ya Tanzania na washiriki wa biashara ili kutambua mazao na bidhaa mbalimbali zinazohitajika kwa wingi katika nchi hizo;

Kuratibu zoezi la ukaguzi wa ubora na usalama wa asali kwa Kampuni 22 kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa ya nchini Saudi Arabia. Kampuni zitakazokidhi viwango vya ubora unaohitajika zitaunganishwa na wanunuzi wa nchini humo ambao wapo tayari kununua asali kutoka Tanzania Kuhamasisha, kushauri na kuelimisha wafanyabiashara wadogo kutumia fursa ya kuuza bidhaa kimtandao kupitia maduka mtandao yanayoratibiwa na Taasisi mbalimbali ikiwemo Shirika la Posta Tanzania (posta e-shop), JD.com

Utoaji wa elimu kuhusu masoko

la China na Food la Saudi Arabia ili kupanua wigo wa kuuza bidhaa za Tanzania nje ya nchi. Mpaka sasa jumla ya wataanzania 350 wanatumia fursa hizo.

IDADI YA WAFANYABIASHARA WALIOPEWA ELIMU KUHUSU MASOKO

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade anasema mamlaka hiyo imefanikiwa kuratibu programu tisa za mafunzo kwa wafanyabiashara ili kuimarisha uwezo wa kujiendesha kiushindani na kutumia ipasavyo fursa za masoko zinazopatikana.

Kupitia program hizo wafanyabiashara na wadau wa biashara wapatao 8,372 walipewa mafunzo mbalimbali yaliyohusu masuala ya masoko na usimamizi wa biashara na waliunganishwa na Taasisi saidizi za kibiashara

ili kupata huduma kama vile usajili wa Kampuni, mikopo na viwango vya bidhaa.

Anasema program hizo ziliratibiwa kwa kuzingatia mahitaji

ya makundi ya wafanyabiashara wakiwemo Wakulima, wajasiriamali, wachimbaji na wasindikaji wa bidhaa katika mikoa mbalimbali nchini.

Jedwali Na.5: Program za Mafunzo zilizoratibiwa mwaka 2021-2023

s/n	Aina ya Mafunzo	Idadi	Mikoa	Matokeo ya Mafunzo
1.	Mbinu za ufungashaji bora (branding) kwa bidhaa za vyakula ikiwemo nafaka na viungo	3,529	Morogoro, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Pwani, Manyara na Shinyanga	Kufahamu mbinu ubora za ufungashaji ili kupunguza upotevu baada ya kuvuna au kusindika; na kuwezesha kampuni kuboresha rajamu za bidhaa kama vile <i>Nguvu Rice, G2L rice, Katani Rice, Tarmo Rice, Ruaha rice</i> , Korie rice na Kibu Rice kwa lengo la kujitangaza kiushindani
2.	Taratibu za uuzaji mazao ya nafaka kwa masoko ya EAC	67	Iringa na Morogoro	Mbinu za mafunzo ziliwawezesha Kampuni za Kibu Agribusiness na Ruaha Milling kuuza mchele wenye thamani ya Sh. 1.3 bilioni katika soko la Kenya na Uganda. Kadhalika, wamefanikiwa kuanzisha Ofisi za uwakala katika nchi hizo ili kurahisha ufanyaji biashara
3.	Taratibu za ufanyaji biashara ya mipakani	88	Mipaka ya Tunduma, Kasumulu na Holili	Kuwezesha Wafanyabiashara Wanawake kufahamu taratibu za kusafirisha bidhaa, kuvuka mipaka kibiashara na kutumia fursa ya unafuu wa taratibu zilizorahisishwa (STR)
4.	Taratibu za kuuza na kuingiza bidhaa ndani na nje ya nchi (Tanzania Trade Portal)	938	Zanzibar, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Dodoma	Kufahamisha wafanyabiashara taratibu na upatikanaji wa vibali vya kuuza (exports), kununua (imports) na kupisha (re-export) ya bidhaa zilizozanishwa kwenye mfumo wa taratibu za biashara (Tanzania Trade Portal). Mfumo una jumla ya watumiaji 16,688 na watembeleaji 45,576 kutoka ndani na nje ya nchi ikiwemo Marekani, Uganda, India, Kenya,

				Afrika Kusini, China, Malawi, Ujerumani, Zambia na Uingereza
5.	Teknolojia ya uchakataji, ubora uongezaji thamani wa dagaa na mwani	450	Unguja na Pemba	Kuhamasika na matumizi ya teknolojia ya uchakataji na uongezaji thamani ya dagaa na mwani ili kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa masoko ya ndani na nje ya nchi
6.	Mbinu za masoko na usimamizi wa biashara	509	Njombe, Songwe, Morogoro na Dar es Salaam	Kufahamu mbinu za kutafuta masoko, kuuza bidhaa kiushindani pamoja na usimamizi wa biashara kwa wadau wanaofanya biashara ya parachichi, mlonge, viungo na bidhaa zilizosindikwa.
7.	Taratibu na Sheria za Ushiriki wa Maonesho ya kibiashara	319	Dar es Salaam	Kuwafamaisha mbinu za ushiriki wa maonesho ili kuweza kujitangaza kwa tija kibiashara ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano na kusaini mikataba.
8.	Program ya urithi kwa wanafunzi wa Sekondari ili kufahamu masuala ya biashara	79	Zanzibar, Lindi, Manyara na Dae es Salaam	Mfunzo kwa vitendo juu ya ujasiriamali na majukumu ya Taasisi Umma, Kimatatifa na Binafsi kupitia maonesho
9.	Kliniki ya Biashara	593	Zanzibar, Dar es Salaam, Geita, Pwani	Kupokea na kutatua changamoto za wafanyabiashara wadogo kuhusu upatikanaji wa mtaji, lesseni, vifungashio, masoko na taratibu za usajili wa jina na alama ya biashara, kemikali na taratibu za kupata vibali mbalimbali vya kufanya biashara za mazao mbalimbali.



Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Doto Biteko akipata maelezo kutoka Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Madini Tanzania STAMICO wakati alipotembelea katika banda hilo kwenye hafla ya ufunguzi wa maonesho ya madini yanayofanyika kwenye viwanja vya Bombabili mjini Geita.